

Nauli mpya daladala, mabasi kuanza kutumika mwezi ujao

Na Mwandishi Wetu

MAMLAKA ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA) imetangaza ongezeko la nauli za mabasi ya masafa marefu, mabasi ya mijini (daladala), teksi mtandao na pikipiki mtandao.

Taarifa ya Mwenyekiti wa bodi Latra, Ahmed Ame imeeleza mamlaka hiyo imetangaza ongezeko hilo chini ya kifungu cha 19 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini, Sura ya 413.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo kupitia Gazeti la Serikali, Latra imefanya mapitio ya viwango vya nauli za vyombo vya usafiri ardhini, na kwamba nauli mpya zitaanza kutumika siku 14 tangu tarehe ya kutangazwa kwa taarifa hiyo Aprili 17, mwaka huu.

"Latra itafuatilia utekelezaji wa viwango vya nauli vilivyowekwa katika taarifa hii ili kuhakikisha kuwa mtoa huduma hatizi nauli inayozidi kiwango kilichowekwa katika taarifa hii," ameeleza Ame.

Nauli za daladala

Tangazo limeeleza mabasi ya mijini (daladala) kwa umbali usiozidi kilometa 10 nauli ni Sh 700, kuanzia kilometa 11 hadi 15 nauli Sh 800, kuanzia kilometa 16 hadi 20 nauli Sh 900, kuanzia kilometa 21 hadi 25 nauli Sh 1,000, kuanzia kilometa 26 hadi 30 nauli Sh 1,200, kuanzia kilometa 31 hadi 35 nauli Sh 1,400 na kuanzia kilometa 36 hadi 40 nauli Sh 1,500.

"Nauli ya mwanafunzi kwa mabasi ya mijini (daladala) kwa umbali wa njia zote itaendelea kuwa Shilingi 200 kwa kila safari," imeeleza Latra.

Nauli masafa marefu

Latra imetangaza kwa safari za masafa marefu nauli za mabasi ya kawaida zitakuwa Sh 57.93 kwa kilometa za barabara za lami na Sh 66.62 kwa kilometa barabara za vumbi.

Kwa mabasi ya kiwango cha kawaida nauli zitakuwa Sh 74.18

kwa barabara za lami.

Nauli za teksi mtandao

Latra imeeleza teksi mtandao zenye uwezo wa kubeba abiria wasiozidi wanne kwa safari isiyozidi kilometa moja nauli ya kiwango cha chini itakuwa Sh 4,000 na kiwango cha juu Sh 5,000.

Nauli ya kuanzia safari (kwa tripu) kiwango cha chini ni Sh 1,100 na Sh 1,200 kiwango cha juu.

Nauli kwa kilometa kiwango cha chini ni Sh 1,100 na Sh 1,300 kiwango cha juu. Nauli kwa dakika kiwango cha chini ni Sh 120 na Sh 150 kiwango cha juu na kamisheni ni asilimia 10 kiwango cha chini na asilimia 20 kiwango cha juu.

Kwa teksi mtandao zenye uwezo wa kubeba abiria zaidi ya wanne nauli kwa safari isiyozidi kilometa moja kiwango cha chini itakuwa Sh 6,000 na Sh 7,000 cha juu.

Nauli ya kuanzia safari (kwa tripu) kiwango cha chini itakuwa Sh 1,300 na kiwango cha juu Sh 1,500. Nauli kwa kilometa kiwango cha chini itakuwa Sh 1300 na kiwango cha juu Sh 1500.

Pikipiki mtandao

Nauli za pikipiki mtandao za magurudumu mawili zikibeba abiria mmoja kiwango cha chini itakuwa Sh 1,500 na kiwango cha juu Sh 2,000.

Nauli ya kuanzia safari (kwa tripu) kiwango cha chini itakuwa Sh 400 na Sh 500 kiwango cha juu na kwa kilometa moja kiwango cha chini itakuwa Sh 400 na kiwango cha juu Sh 500.

Kwa pikipiki mtandao za magurudumu matatu zikibeba abiria wasiozidi watatu nauli kwa safari isiyozidi kilometa moja kiwango cha chini itakuwa Sh 3,000 na Sh 4,000 kiwango cha juu.

Nauli ya kuanzia safari (kwa tripu) kiwango cha chini itakuwa Sh 500 na Sh 700 kiwango cha juu na kilometa moja nauli kiwango cha chini itakuwa Sh 700 na kiwango cha juu Sh 900.